


# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI VETA KIGOMA

## KIGOMA RVTSC



### MAELEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NGAZI YA KWANZA (LEVEL I), 2025

#### 1. Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako chuoni.

- a. Mashati mawili meupe (mikono mifupi) ya tetroni.
- b. Jozi ya viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi
- c. Viatu vya usalama kwenye karakana.



- d. Vifaa vya hesabu (mathematical set). Viatu Vyeusi
- e. Daftari 6 kubwa.
- f. Nguo za michezo t/shirt na bukta rangi ya blue na raba.
- g. Unatakiwa kuja na Picha 2 za passport size, picha izingatie yafuatayo:-
  - i. Shati liwe jeupe
  - ii. iwe na background ya blue maji bahari.
- h. Sweta moja rangi ya blue (Takron)
- i. Ream moja ya karatasi A4 na ikabidhiwe kwa Msajili

#### 2. Gharama nyingine ni kama inavyosomeka kwenye jedwali hapo chini:-

Mwanafunzi wa Kutwa (Day Scholar)				
Namba	Mahitaji	Idadi	Kiasi	Jumla
1.	Ada ya mafunzo		60,000	60,000
2.	Nembo	2	3,000	6,000
3.	Fulana	1	15,000	15,000
4.	Kitambulisho (Identity card)	1	10,000	10,000
5.	Fedha za uchakavu/ukarabati	1	20,000	20,000
6.	Michezo	1	10,000	10,000
7.	Suruali mbili rangi ya blue	2	20,000	40,000
8.	Overcoat/overall	1	30,000	30,000
9.	Mahafali	1	10,000	10,000
<b>JUMLA (Wanafunzi wa Kutwa)</b>				<b>201,000</b>

Mwanafunzi wa Bweni (Boarding Scholar)				
Namba	Mahitaji	Idadi	Kiasi	Jumla
1.	Ada ya mafunzo		120,000	120,000
2.	Nembo	2	3,000	6,000
3.	Fulana	1	15,000	15,000
4.	Kitambulisho (Identity card)	1	10,000	10,000
5.	Fedha za uchakavu		20,000	20,000
6.	Michezo		10,000	10,000
7.	Suruali mbili rangi ya blue	2	20,000	40,000
8.	Overroll/overcoat	1	30,000	30,000
9.	Kukodi godoro (mwanafunzi wa bweni)	1	10,000	10,000
10.	Mahafali		10,000	10,000
11.	Bima ya Afya (mwanafunzi wa bweni asiyekuwa na bima)		50,400	50,400
<b>JUMLA (Wanafunzi wa bweni asiyekuwa na Bima ya Afya)</b>				<b>321,400</b>
<b>JUMLA (Wanafunzi wa Mwenye Bima ya Afya)</b>				<b>251,400</b>

- a) Malipo yote ispokuwa malipo ya bima yafanyike kwa kutumia mfumo wa malipo wa serikali kwa kutumia **control namba utakayopewa chuoni**.
  - b) Malipo ya Bima yatapelekwa moja kwa moja NHIF kwa utaratibu utakaopewa chuoni. **NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIDA) ni muhimu sana kuja nayo.**
  - c) Kumbuka kuandika **jina kamili la mwanafunzi** kwenye slip ya malipo ya benki.
  - d) Slip hiyo lazima ikabidhiwe kwa msajili mara tu mwanafunzi anaporipoti chuoni.
3. Kwa mwanachuo aliyepatiwa nafasi ya bweni, aje na mto, shuka, blanketi, chandarua, bakuli, sahani, kikombe na kijiko pamoja na ndoo au beseni la kuogea pamoja na vifaa vya usafi binafsi.
  4. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Fedha ikishalipwa hairudishwi.
  5. Siku unaripoti unatakiwa kuja na cheti chako halisi kwa ajili ya uthibitisho wa kiwango chako cha Elimu.
  6. Utalazimika kulipia Ada ya mitihani ya Taifa Elfu Ishirini (25,000/-) Mwezi Agosti au utakapojulishwa.
  7. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatishwa kwenye barua hii.
  8. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza Mafunzo.
  9. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti ndani ya **WIKI MBILI** baada ya tarehe ya kufungua chuo.

Paul Kimenya Titus  
**KAIMU MKUU WA CHUO**

## SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

Kwa muda wote Mwanachuo unapokuwepo chuoni unatakiwa kufuata taratibu na sheria za chuo. Kutokufanya hivyo kunaweza kupelekea hatua kali za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yako. Zifuatazo ni taratibu na sheria za chuo:-

### 1. MAHUDHURIO

- (a) Kila mwanachuo anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1.30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1.30 asubuhi wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni.
- (b) Mwanachuo hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote kwa sababu ya msiba, kuuguliwa au kuugua ni lazima apate kibali cha Mkuu wa chuo.
- (c) Mahudhurio chini ya 85% mwanachuo hataruhusiwa kufanya mtihani.
- (d) Ni Marufuku kwa mwanachuo kuingia au kutumia simu ya mkononi sehemu yoyote inayohusiana na mafunzo ikiwa ni darasani au kwenye karakana.

### 2. MAVAZI NA USAFI WA MWILI

- (a) Mwanachuo unatakiwa kuvaa sare ya chuo ambayo ni suruali ya bluu yenye vipimo vilivyothibitishwa na chuo wakati wote unapokuwa katika mazingira ya chuo. Shati jeupe la mikono mifupi lenye nembo ya VETA lililo chomekewa vizuri ndani ya suruali. Mwanachuo atakayevaa sare ya chuo isiyokidhi vipimo atalazimika kushona/kununua nyingine.
- (b) Sare ya chuo itavaliwa wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Ovaroli litavaliwa wakati wa vipindi vya mazoezi kwa vitendo.
- (c) Viatu vyenye visigino virefu, kandambili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni wakati wa mafunzo.
- (d) Hairuhusiwi kuvaa mapambo ya aina yoyote ile mfano hereni, pete, bangili, mkufu kwa kipindi chote cha mafunzo.
- (e) Mwanachuo huruhusiwi: kupaka rangi za midomo, kuweka dawa/rangi za nywele, manukato yanayotoa harufu kali, kufuga kucha au kuzipaka rangi, kuvaa bangili, hereni, mkufu, au urembo wowote.
- (f) Nywele kwa wavulana:  
Zikatwe ziwe fupi na isiwe kipara. Hairuhusiwi kunyoa mitindo mingine na kufuga sharubu au ndevu.
- (g) Nywele kwa wasichana:  
Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma (twende kilioni). Hairuhusiwi kunyoa au kusuka mitindo nje ya iliyoruhusiwa.

**3. USAFI WA MAZINGIRA YA CHUO**

- i) Mwanachuo unatakiwa kutunza usafi wa mazingira ya chuo ikiwa ni pamoja na kutoandika katika kuta za majengo na kutokukatisha katika sehemu isiyoruhusiwa hasa katika bustani za nyasi.
- ii) Mwanachuo huruhusiwi kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo, wala kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.
- iii) Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake, hairuhusiwi kupeleka meza au viti mabwenini.

**4. WIZI, UPOTEVU NA UHARIBIFU WA VIFAA:**

- (a) Vitendo vyovyote vinavyohusisha wizi ni kosa la jinai.
- (b) Ukipoteza au kuharibu kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa au ukakinunue kifaa chenyewe.
- (c) Ni kosa kubwa kung'oa taa kwa lengo la kuiba au kuhamishia sehemu nyingine bila kibali
- (d) Hairuhusiwi mwanachuo kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo bila idhini ya mkuu wa chuo.
- (e) Mwanachuo atapekuliwa au kukaguliwa wakati wa kutoka au kuingia karakana na getini.

**5. UGOMVI**

Kupiga, kupigana na kushambuliana kwa maneno ni makosa ya jinai.

**6. ULEVI**

Mwanachuo haruhusiwi kulewa au kuonekana katika sehemu za vileo, kuvuta bangi au kutumia madawa ya kulevya.

**7. MAPENZI:**

- (a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya Wanachuo au kati ya mfanyakazi na mwanachuo hauruhusiwi kabisa.
- (b) Mwanachuo yeyote haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

**8. MIGOMO:**

Kushiriki, kushawishi au kuchochea migomo ni kosa la jinai, hivyo hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.

## JEDWALI LA MAKOSA MBALIMBALI NA ADHABU ZAKE

Na.	MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA CHUO	MAKOSA YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA MASOMO/ KUNYANG'ANYWA NAFASI YA BWENI	MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUPELEKEA KUPEWA ADHABU
	<ul style="list-style-type: none"> <li>a) Wizi, rushwa na utapeli.</li> <li>b) Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji bangi.</li> <li>c) Kupiga au kupigana.</li> <li>d) Ubakaji na ushoga chuoni.</li> <li>e) Kudharau bendera ya Taifa.</li> <li>f) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo, kuvuruga amani na usalama wa Chuo na watu.</li> <li>g) Kufanya jaribio lolote la kujiua/kuua.</li> <li>h) Kushiriki vitendo vya ugaidi.</li> <li>i) Utoro uliokithiri.</li> <li>j) Kumlaza mgeni bwenini.</li> <li>k) Kupika chakula /kutumia "heater" bwenini.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>a) Kukataa adhabu halali.</li> <li>b) Kuharibu mali ya chuo.</li> <li>c) Uasherati</li> <li>d) Kutofanya mitihani/mazoezi bila sababu.</li> <li>e) Kufanya biashara na kujihusisha na siasa chuoni.</li> <li>f) Kuingia na mgeni/kumkaribisha mgeni bwenini.</li> <li>g) Kutumia vifaa visivyoruhusiwa bwenini.</li> <li>h) Kulala nje ya chuo bila ruhusa ya mkuu wa chuo.</li> <li>i) Kutumia lugha ya matusi.</li> <li>j) Kutovaa sare ya chuo awapo nje ya chuo.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>a) Kuingia maeneo yasiyoruhusiwa.</li> <li>b) Kuingia na kifaa chochote kile kinacho fanana na vilivyoko ndani ya chuo bila ruhusa.</li> <li>c) Kupeleka meza au viti bwenini.</li> <li>d) Kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo, kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.</li> <li>e) Kutotunza usafi wa mazingira ya chuo.</li> <li>f) Kukatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.</li> <li>g) Kutozingatia usafi wa mwili.</li> <li>h) Kutoka nje ya chuo bila ruhusa.</li> <li>i) Kuchelewa kuripoti chuoni kabla ya saa 1.30 asubuhi</li> <li>j) Kupoteza kifaa cha chuo.</li> </ul>

**SHERIA ZA ZIADA KWA MWANACHUO WA BWENI**

1. Mwanachuo unaruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo tu:-
  - a) Jumamosi kuanzia saa 4.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni
  - b) Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni.
2. Mwanachuo mwenye kibali/ruhusa ya kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa na sare ya Chuo, kitambulisho cha Chuo na atajiandikisha lango kuu.
3. Mwanachuo huruhusiwi kulala au kuwa nje ya chuo bila kibali
4. Hairuhusiwi kupika chakula bwenini/kutumia “heater” eneo la chuo.
5. Ni marufuku kwa mwanachuo wa kiume na wa kike kutembeleana mabwenini.
6. Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu/mlezi wa bweni itatolewa.
7. Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:00 usiku.
8. Hairuhusiwi kumkaribisha au kumlaza mgeni bwenini. Hairuhusiwi kutembelewa na wageni siku za masomo, Ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni siku ya masomo ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo. Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea wanachuo siku zifuatazo:
  - a) Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni, na
  - b) Jumapili na sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka 12:00 jioni.

**Paul Kimenya Titus**  
**KAIMU MKUU WA CHUO**

MEDICAL INTRODUCTION LETTER

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

Tel. +255 28 2988169

Email: [kigomarvtsc@veta.go.tz](mailto:kigomarvtsc@veta.go.tz)

Website: [www.veta.go.tz](http://www.veta.go.tz)



KIGOMA RVTSC

P. O. Box 1068,

KIGOMA.

Date: ...../...../ 2025.

The Medical Officer

.....  
.....  
.....

**RE: MEDICAL EXAMINATION FORM**

Name of trainee .....

Please examine the above named trainee to his/her fitness to undergo vocational training and subsequently work as.....

With this letter, please find the attached medical examination form.

The form consists of section A and B; Section A to be completed by the applicant interviewed by the registered medical Officer; and Section B to be completed by a registered medical Officer. The completed form must be submitted to the Centre by the trainee together with all other application materials.

Yours,

.....  
Paul Kimenya Titus  
AG.PRINCIPAL

**SECTION A:**

**(TO BE COMPLETED BY THE APPLICANT)**

**Full Name:** .....**Date of Birth:** .....

**Marital Status:** .....**Gender:** .....

**Occupation:** .....

<p><b>(i) NERVOUS SYSTEM</b></p> <p>Any loss of consciousness? YES/NO If Yes dates of Incident .....</p> <p>Current treatment: .....</p> <p>Any Neurological deficiency? Yes/No If Yes, state deficiency: .....</p> <p>When acquired: .....</p> <p>Current treatment: .....</p> <p>Any fits? Yes/No If Yes types of fits: .....</p> <p>Date of last episode: .....</p> <p>Current treatment: .....</p> <p><b>(ii) MUSCULOR SKELETAL SYSTEM</b></p> <p>Any Deformity? Yes/No If Yes, which part of Body: .....</p> <p>When acquired: .....</p> <p>Use of accessories or aids: .....</p> <p><b>(iii) OTHER CHRONIC CONDITIONS</b></p> <p>Diabetes Mellitus? Yes/No If Yes, when detected .....</p> <p>Current Status .....</p> <p>Tuberculosis? Yes/No If Yes, When detected: .....</p>	<p>Herpes Zoster? YES/NO If Yes, Date of illness: .....</p> <p>Part of body affected: .....</p> <p>Hypertension? Yes/No If Yes, when detected: .....</p> <p>Current treatment: .....</p> <p>Asthma? Yes/No If Yes when detected: .....</p> <p>Current treatment: .....</p> <p>Allergies? Yes/No If Yes date of last reaction: .....</p> <p>Cause of reaction: .....</p> <p>Major surgeries? Yes/No If yes, type of surgery: .....</p> <p>Outcome of surgery: .....</p> <p>Any heart disease? Yes/No If Yes, what disease? .....</p> <p>Current treatment: .....</p> <p>Any Dietary Restrictions? Yes/No If Yes state restriction: .....</p> <p>Please Note: The applicant is responsible for maintaining any dietary restrictions.</p>
---	--

<p><b>(iv) DECLARATION</b></p> <p>I Declare that all the information provided therein is true to the best of my knowledge.</p> <p><b>Signature:</b> ..... <b>Date:</b> .....</p>
--



**SECTION B:**

**(TO BE COMPLETED BY REGISTERED MEDICAL OFFICER)**

**Full Name of the trainee (applicant):** .....

<b>v) VARIOUS TESTS</b>	
<b>A. GENERAL APPEARANCE</b> Height: ..... Weight: ..... Blood Pressure: ..... Pulse Rate: ..... Lymph node Palpable ..... Skin appearance: ..... Throat Tonsils: ..... Teeth Dentition: ..... Carious: .....	<b>B. MUSCULLOR SKELETAL SYSTEM</b> Any deformation? Yes/No If Yes which part of the body: ..... Type of deformity: .....
<b>EARS</b> Rt Hearing ..... Drum Membrane: ..... Lt Hearing: ..... Drum Membrane: .....	
<b>EYES</b> Rt VA: ..... Squint: ..... Lt: VA: ..... Squint: .....	
<b>C. OTHER OBSERVATIONS</b> Any other observations whether irritable or aggressive	
<b>D. DECLARATION</b> ID ..... of ..... Has examined the named ..... Candidate and conclude that the candidate is/is not suitable to attend one/two/three year programme at ..... College. <b>Signature with Official Stamp:</b> ..... <b>Date:</b> .....	

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI



FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

a) MWANACHUO

Mimi .....ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na taratibu za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Saini.....Tarehe.....

b) MZAZI/MLEZI/MDHAMINI

Mimi..... ambaye ni Mzazi/Mlezi/Mdhaminiwa mtajwa hapo juu nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na michango mingine wakati wote wa mafunzo kama ilivyoelekezwa katika fomu ya kujiunga na chuo.

Saini.....Tarehe .....

Namba ya simu .....